**REPUBLIC OF KENYA**

**MINISTRY OF ENVIRONMENT AND NATURAL RESOURCES**
**STATE DEPARTMENT OF ENVIRONMENT**
**KENYA METEOROLOGICAL DEPARTMENT**
Dagoretti Corner, Ngong Road, P. O. Box 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya
**Telephone:** 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4 **E-mail:** director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke;
**Website:** http://www.meteo.go.ke


***When replying please quote***
**Our Ref:** Met/7/43 **Date:** 29th August 2017

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU**
**TATHMINI YA MSIMU WA MVUA ZA VULI – OKTOBA-NOVEMBA-DISEMBA (OND) 2017**

***Namba ya Kumbukumbu: KMD/UTABIRI/ 5-2017/SO/03***

***Tarehe: 29/08/2017***

## 1. MUKHTASARI

### Utabiri wa Oktoba-Novemba-Desemba (OND) 2017

Matazamio ya msimu wa Oktoba-Novemba-Desemba (OND) 2017 "Mvua za Vuli" yanaonekana mazuri kiasi ya kwamba maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na mvua ya kutosha.

Sehemu zinazotarajiwa kuwa na mvua nyingi ni kama maeneo yote ya kaskazini mwa nchi, majimbo yote ya kati mwa nchi, mji wa Nairobi na maeneo ya mwambao wa pwani.

Majimbo ya magharibi mwa nchi, na tambarare za kusini mashariki mwa nchi mvua inatarajiwa kuwa ya kiwango cha kawaida.

Mvua ya msimu katika maeneo mengi itaanza kati ya wiki ya pili na tatu ya Oktoba na kutamatika wiki ya tatu ya Disemba. Mgawo wa mvua za vuli unatarajiwa kuwa mzuri. Kunatarajiwa kuwa na vipindi virefu vya ukame mwezi wa Disemba. Kama kawaida ya msimu huu, Novemba ndiyo inatazamiwa kuwa kilele cha mvua ya msimu.

Tathmini hii ya mvua za Vuli umefanywa kulingana na takwimu na taratibu za kisayansi, pamoja na vile hali ya joto inavyobadilika katika bahari ya Hindi.

## 2. Utabiri wa hali wa Mvua za Vuli kwa Kina

Msimu wa Oktoba-Novemba-Disemba ni muhimu sana Kenya na Africa Mashariki kwa ujumla. Msimu huu unajulikana kama "Mvua za Vuli ama kipindi cha mvua fupi".

Msimu huu ni muhimu hususan maeneo ya mashariki mwa nchi ambapo ndio msimu peke wakulima hupata mavuno mazuri ukilinganisha na msimu wa masika (Machi-Aprili- Mei).

**Utabiri wa msimu wa mvua za Vuli ni kama ufuatavyo**: (***Ramani namba 1 chini)***

i. Majimbo yalioko magharibi mwa nchi **(Busia, Bungoma, Vihiga, na Kakamega, )**, na yale yanayopakana na Ziwa Victoria - majimbo ya Nyanza **(Kisumu, Siaya, Homa Bay, Nyamira, Migori, Kisii,..)**;pamoja na majibo ya bonde la ufa kusini, kati na kaskazi; (**Kericho, West Pokot, Nandi, Bomet, Baringo Uasin Gishu, Trans Nzoia, Nakuru, Narok Kajiado**); Majimbo ya kusini mwa nchi kama **(Taita-Taveta, Machakos, Makueni, Kitui na sehemu kubwa ya Tana River); na Nairobi** yatapokea mvua ya kiwango cha kawaida ya msimu huu;

ii. Majimbo ya Kati na mashariki mwa nchi **(Nyeri, Kiambu, Murang'a, Kirinyaga na Nyandarua, Meru, Embu na Tharaka**)**;** majimbo ya mashariki mwa nchi; (sehemu ya kaskazini ya **Kitui, Wajir, Isiolo, Garissa,Marsabit, Moyale**); mwambao wa Pwani (**Kwale, Mombasa, sehemu ndogo ya Tana River, Kilifi, Lamu**); na majimbo ya kaskazini mwa nchi **(Samburu, Isiolo, Laikipia, na Turkana, Mandera,..**) yanatarajiwa kupata mvua ya kutosha na hata sehemu zingine kuwa nyingi.

**3. Mvua Inayotarajiwa kuanza na kumalizika kama ifuatavyo: Angalia Ramani namba 2 na 3 chini**

- Majimbo ya Nyanza and Magharibi (Kisumu, Siaya, Homa Bay, Nyamira, Migori, Kisii, Busia, Vihiga, Kakamega, Bungoma nk..): Sehemu hizi kwa sasa zinapata mvua kidogo. Itaongezeka kuanzia wiki ya kwanza Oktoba 2017. Mvua inatarajiwa kutamatika *Kati ya Wiki ya 4 Disemba 2017*
- Majimbo ya Uasin Gishu, Trans Nzoia: Mvua inatarajiwa kuanza huko maeneo ya Kitale, Eldoret mnamo wiki ya pili Oktoba na kuisha wiki ya kwanza hadi wiki ya pili Disemba.
- Majimbo ya Kaskazini mwa Bonde la Ufa: (Turkana, West Pokot counties ) mvua itaanza wiki ya nne Oktoba na kukatika wiki ya kwanza Disemba;
- Majimbo ya Kati mwa Nchi: Nyanda za Juu (Meru, Embu, Nyeri, Murang'a, Laikipia): maeneo haya yantarajiwa kuanza kupata mvua wiki ya pili hadi ya tatu Oktoba. Mvua itakatika wiki ya pili hadi ya tatu Disemba;
- Jimbo la Nairobi na sehemu tambarare za kusini (Dagoretti, Kabete, Eastleigh, Machakos, Kangundo,): Mvua itaanza wiki ya tatu hadi nne ya Oktoba na kuisha wiki ya pili hadi tatu ya Disemba.
- Majimbo ya Kaskazini mashariki (Mandera, Wajir, Garissa, Marsabit): Mvua inatarajiwa kuanza wiki ya pili hadi ya tatu ya Oktoba na kuisha wiki ya nne Novemba hadi ya kwanza Disemba. Disemba huenda ikawa kavu
- Majimbo ya Bonde la Ufa la kati: (Nakuru, Narok, Nyahururu etc) : Mvua itaanza wiki ya tatu hadi nne ya Oktoba na kuisha wiki ya kwanza hadi ya pili ya Disemba. Jimbo la Narok huenda likapata mvua hadi mwisho wa mwezi wa Disemba mpaka Januari mwakani.
- Maeneo ya Kusini mwa nchi: (Taita Taveta, Makueni, sehemu ya kusini mwa Tana River) mvua inatarajiwa kuanza wiki ya nne Oktoba na kukatika wiki ya tatu hadi ya nne Disemba.
- Mwambao wa Pwani ( Mombasa, Kilifi, Kwale na Lamu) mvua inatarajiwa kuanza wiki ya pili hadi ya tatu Oktoba na kukatika wiki ya kwanza hadi ya pili Disemba.

**4. Matarajio ya Mgawo wa Mvua ya Msimu**

Mgawo wa mvua wa Mvua za Vuli 2017 unatarajiwa kuwa mzuri katika maeneo mengi ya nchi. Kuna uwezekano kuwepo na kipindi kirefu kikavu ndani ya msimu hasa mwezi wa Disemba. Hata hivyo bado mwezi wa Novemba unatarajiwa kuwa kilele cha mvua ya msimu.

## 5. Sekta Mbalimbali za Uchumi Zitakazo Athiriwa na Mvua ya Msimu wa Vuli (Oktoba-Novemba-Disemba)

Hali ya hewa inaathiri sekta karibu zote za uchumi kutokana na ile hali ya kuwa rasimali nyingi zinatokana na wingi ama upungufu wa mvua za msimu. Hapa tunajaribu kutathmini vile sekta zifuatazo zitakavyoathirika:

### 5.1 Sekta ya Kilimo, Chakula na Ufugaji wa Mifugo

- Msimu huu vua ya inatarajiwa kuwa ya kutosha katika maeneo mengi ya kilimo nchini. Pia inatarajiwa, na mgawo pia unatarajiwa kuwa mzuri. Hali hii itafaidi shughuli za kilimo katika maeneo mengi. Wakulima wanashauriwa kushirikiana na maafisa wa Wizara ya Kilimo ili wajulishwe vile watavyofanya kufaidi zaidi mvua, kwa kuchagua mimea inayofaa kukuzwa ili kuzalisha mazao mengi.
- Malisho na maji ya mifugo katika maeneo ya ufugaji yataongezeka.

### 5.2 Mazingira

Kutokana na mvua nzuri ambayo inatarajiwa katika maeneo mengi, ni wakati mzuri wa kuboresha mazingira yetu kwa kupanda miti kwa wingi. Wananchi wasitishe kutumia mifuko ya plastiki ambayo wakati mwingi inatupwa ovyo na kuharibu mandhari ya nchi yetu. Mitaro na mashimo yanaweza kuweka maji wakati huu wa mvua. Ni muhimu kujaza mashimo ili kuepuka maji kusimika na kuzalisha umbu.

### 5.3 Sekta ya Maji

Kuna uwezekano mkubwa hali ya maji kuregea kawaida kutokana na mvua nyingi inayotarajiwa kunyesha katika vianzio vya mito hasa sehemu za Nairobi, Nakuru, Mombasa, Garisa, Eldoret,nk. Wananchi wanahimizwa kutega maji ya mvua na kuyahifadhi kwa matumizi wakati wa ukosefu wa bidhaa hiyo badaye.

### 5.4 Kitengo kinachokabiliana na Majanga (NDOC)

1. Kuna uwezekano wa kutokea upotovu wa usalama baina ya wafugaji kutokana na haja ya kuongeza mifugo kufidia iliyokufa wakati wa kipindi cha ukame. Vyombo vinavyohusika na usalamu ni muhimu vifwatilia hali inavyojiri kwa makini ili kutibua njama na kupunguza mathara.
2. Huko maghaibi mwa nchi- Kisii, Kisumu, Kakamega and Mlima Elgon, kutokana mvua ya ngurumo na radi, ni muhimu watu watahadharishwe na uwezekano wa kupigwa na radi.
3. Hata maeneo ambayo hupata mafuriko kila mara kunyeshapo, mikakati kabambe iwekwe kukabiliana na hali hiyo.

### 5.5 Sekta ya Afya

Magonjwa yanayosababishwa na wingi wa mvua na ukosefu wa mazingira safi kama vile homa ya matumbo na kipindupindu yanaweza kujitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo yanatarajiwa kupata mvua nyingi. Maafisa wa Wizara ya Afya na Huduma za Kimatibabu wanashauriwa kuwa macho juu ya kesi kama hizo. Kuna haja ya Hospitali kufanya mipango mapema kuwa na vifaa na madawa muhimu ili kukabiliana na hali kama hizi zinapojitokeza.

**5.6 Usafiri na Sekta ya Usalama wa Umma**

Kutokana na mvua nyingi inayotarajiwa baadhi ya maeneo ya nchi, kuna uwezekano wa kuwa na hali ya mafuriko na barabara kuwa telezi. Hii inaweza kusababisha ajali. Serikali za Ugatuzi hasa Mijini zinashauriwa kuzibua mabomba ya maji taka ili kuwezesha maji yapite kwa urahisi kuepuka mafuriko mijini. Madereva pia wanashauriwa kuendesha magari kwa makini ili kuepuka ajali ambazo zinaweza kutokana na hali ya barabara mbaya.

**5.7 Sekta ya Uzalishaji Umeme (Nishati)**

Kuna uwezekano mkubwa wa kupata mvua ya kutosha katika maeneo ya vyanzio vya mito mikubwa, kama Sondu Miriu, Tana na Athi, inayomimina maji yake kwa mabwawa ya kuzalisha umeme. Uwezo wa uzalishaji wa umeme katika mabwawa haya huenda ukaimarka kwa kiasi kikubwa. Kuna umuhimu wa taasisi za kuzalisha umeme kufuatilia, kwa makini, utabiri wa msimu ili kutumia mbinu muafaka za kutumia maji kwa ajili ya kuepuka ukosefu wa nguvu za umeme kwa matumizi ya viwanda na nyumbani.

**6. Ilani:**

**Kumbuka:** utabiri huu lazima kutumiwa pamoja na utabiri unaotolewa kila siku, wiki hata mwezi na Idara hii. Utabiri wa kina kwa majimbo ukutolewa na maafisa wa Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa katika kaunti siku chache zijazo.

**BW, PETER G. AMBENJE**
**MKURUGENZI WA HUDUMA ZA UTABIRI WA HALI YA HEWA NA MWAKILISHI WA KUDUMU WA KENYA KATIKA SHIRIKA LA UTABIRI WA HALI YA HEWA ULIMWENGUNI**

Ramani Namba 1: Utabiri wa msimu wa OND 2017







*Ramani namba 2 wa Tarehe za Mwanzo wa mvua*




*Ramanio namba 3 wa Tarehe za Mwisho wa mvua*